


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI



01 JUNI, 2018

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 01 JUNI, 2018

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**351. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wapo Wahitimu wengi sana kutoka Vyuo mbalimbali vya ufundis nchini ambao hadi sasa hawajapata ajira wala hawajaweza kujiajiri, ikiwa pia tuko kwenye

wakati wa kuanzisha uchumi wa Viwanda ambapo taaluma za Wahitimu hao zitahitajika sana:-

Je, ni lini Serikali itafanya juhudzi za dhati za kulishughulikia suala hili kwa lengo la kuongezatija.

### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **352. MHESHIMIWA LAMECK OKAMBO AIRO (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Rarya iliyoanzishwa mwaka 2007 sasa ina wakazi wapatao 400,000 na ina Kata 26 na Vijiji takriban 87 na ina Vituo vya Afya 4 lakini haina Hospitali ya Wilaya na Wananchi wake hulazimika kutembea umbali wa takriban Km 30 kufuata huduma za afya Tarime na Akina Mama ambao ni asilimia 52 wanahitaji huduma ya Hospitali kamili:-

Je, ni lini Wilaya ya Rarya itajengewa Hospitali ya Wilaya.

### **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

#### **353. MHESHIMIWA JOSEPH ROMAN SELASINI (ROMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Vipo vyanzo vya maji kutoka Mlima Kilimanjaro ambavyo vinasemekana vinapeleka maji nchini Kenya kupitia Msitu wa Rongai:-

Je, Serikali haioni sababu za kudhibiti vyanzo hivyo ili kuhakikisha kwamba maji hayo yanatumika katika Halmashauri ya Rombo badala ya kwenda nchi jirani ya Kenya.

#### **354. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Uhaba wa maji safi na salama imekuwa ni kero kubwa kwa Wananchi wa Wilaya ya Manyoni na Mkoa wa Singida:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha miradi mikubwa ya maji ambayo itahudumia Wananchi wa maeneo hayo muda wote.

#### **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

#### **355. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Moja ya sababu

zinazochelewesha kuanza kwa Mgodi wa Kabanga Nickel ni umeme na reli:-  
Je, ni lini reli ya Isaka – Keza kuelekea Burundi na Rwanda itajengwa.

**356. MHESHIMIWA MAHMOUD HASSAN MGIMWA (MUFINDI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika Kata za Mapanda, Mpangatazara, Ihuru na Ikweha.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**357. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Chuo cha Utalii kimetoa Wahitimu wangapi wa fani za Hoteli za Kitalii kwa mwaka 2016/2017.

**358. MHESHIMIWA SHAABANI OMAR SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wilaya ya Lushoto imezungukwa na misitu lakini misitu mingi imeungua kwa moto:-  
Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha uoto ule wa asili uliopotea kutokana na misitu kuungua.

**359. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED ABDALLAH (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kilwa ni moja ya Miji mikongwe katika Afrika Mashariki tangu Anno Domino (AD) 900 – 1700 pamoja na Miji mingine ya Lamu, Mombasa, Sofala na Zanzibar. Miji hiyo ilipewa heshima ya jina la Urithi wa Dunia (*World Heritage Sight*). Kwa kawaida Miji hiyo husaidiwa na Mataifa mbalimbali ikiwemo Marekani, Japan, Ujerumani, Uingereza na Shirika la UNICEF:-

Je, Serikali ya Tanzania imefaidika nini kutoka katika Mataifa hayo yanayosaidia nchi za urithi wa Dunia.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MADINI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**(Majadiliano yanaendelea)**

**DODOMA**  
**01 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**